

HABARI LEO UK 20.

*Wavuvi wadogo waomba viwanda vya samaki *



**Na Mwandishi Maalumu,
Kilwa**

WAVUVI na wadau wa uvuvi wilayani Kilwa wameomba serikali kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya baharini ili wawe na uhakika na kazi yao.

Kauli hiyo imetolewa katika semina ya wadau wa uvuvi na wavuvi inayofanyika katika mji wa bandari ndogo ya Kilwa Kivinje, wilayani Kilwa mkoani Lindi. Semina hiyo imelenga kujuu hali ilivyo mionganii mwa wavuvi wadogo nchini Tanzania.

Semina hiyo imeandalifi na Wizara ya Maeendeleo ya Mifugo na Uvuvu kwa kushirikiana na wadau wengine katika utekelezaji wa mradi mdogo wa Mwongozo wa

Hiyari wa Kuhakikisha Uendelevu wa Uvuvu Mdogo kwa ajili ya kuhakikisha Usalama wa Chakula na Kuondoa Umaskini kwa ufadhibili wa Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO)..

Mradi huo pamoja na mambo mengine unalenga kuandaa mpango wa kitaifa wa kutekeleza mwongozo huo.

Akizungumza katika kikao hicho mdau wa uvuvi, Omari Mfulule alisema wamekuwa na shida kubwa na soko kwa sababu mbalimbali..

Alisema kama wakipatiwa viwanda watakuwa na uhakika wa soko na kazi ya uvuvi itakuwa nzuri zaidi. Alisema kwa sasa hata eneo la hifadhi ya bidhaa zao halipo na inakuwa kero kwao.

Johari Abdallah alisema

kwamba amefurahishwa na serikali kuamua kusikiliza kilio cha wavuvi na kusema moja ya taabu kubwa ni mifumo ya kuhifadhi bidhaa wakitoka katika hekaheka ya uvuvi.

Aidha alisema ni vyema mnyororo mzima wa uvuvi kuangalia kutatua shida za wavuvi wadogo ili shughuli hiyo isonge mbele wilayani Kilwa na nchini pia.

Naye mfanyakishara wa mazao ya uvuvi, Julius Nyengele alisema wanachoomba wao kama wafanyakishara ni uwepo wa hifadhi nzuri na kupunguziwa tozo.

"Kwa sasa ukichukua dagaa mathalani wale waliokaushwa kwa juu na wale waliochemshwa kwa chumvi na kuanikwa pamoja na thamani moja wanatozwa bei kubwa kwa kuangalia uzito na

inatuletea usumbufu," alisema Nyengele.

Ofisa Uvuvu, Michael Mafundi alisema serikali imeshusha tozo nyangi na zingine kuziondoa katika sekta ya uvuvi kwa lengo la kuifanya ishamiri.

Alisema hata hivyo serikali yenye we hupata tozo zake kwa kuangalia uzito wa mzigio na wala hiyo haiwezi kuwa na usumbufu kwa wadau.

Naye Mkurugenzi wa shirika lisilokuwa la kiserikali la (EMEDDO) linashughulika na usimamizi wa mazingira na maendeleo, Editrudith Lukanga alisema wamefurahishwa na uwapo wa semina ya wadau wa uvuvi na wavuvi ambayo imelenga kubaini changamoto zao na kujuu njia mbadala ya kutatua changamoto hizo.

*Wizara yawashika mkono wananchi Mkuranga kuingia ufugaji wa kisasa

- Vita kuukabili ‘mdondo’, kulinda nyama nyeupe

Na Yasmine Protace, MKURANGA

KATIKA kuwawezesha wafugajj kuku wanusaike na bidhaa yao, kanuni inayotawala ni kwamba kuna kila sababu ya kuwapatia mafunzo, wazalishis kwa vi-wango bora.

Ndani ya mtazamo huo, kuna ukweli unaotawala kwamba wafugaji wanajitokeza zaidi kufuga kuku, lakini wa-naishia katika hasara hasa kutokana na mifugo hiyo kufa.

Ili infugaji aweze kuzalisha kuku bora na wenyewe asya bora, anatakiwa wapatiwe masunzo ya usugaji, kuhakikisha bidhaa hiyo inawainua kiuchumi.
Hadi sasa kuna waufugaji katika mikoa,

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde, anasema kuwa hadi sasa serikali inaendelea kuwapatia mafunzo wafugaji kuku, ili wazalishes idadi kubwa ya mifugo hivo.

Anasema, lengo la mafunzo hayo ni kuhawezesha wazalishe kuku bora na wengi, ili kuchangia kusimama kwa uchumwa nchi, wfugajii wanaendesha shughulzaa kwa tija inavostabilii.

Nandonde anaafanaru kuwa, ana angalizo la kiuchumi kwamba, inapotokee wa fugaji kuku watashindwa kufanya uwekezaji wa nyama nyeupe, inabebazafisri ya athari kuwapo eneo la kiuchumi mi lanalochechemea.

"Tumetoa mafunzo ya siku mbili kwa wafugaji kuku kutoka makundi 30 ambayo yanafuga kuku," anasema na kudokeza kuna schemu ya angalizo la Mpango Kabambe wa Mifugo wa Mwaka 2017 hadi 2021, unaosimamia na wizara venye dhamaani la uvuvi kitaifa.

Anasema mtazamo uliopo hivi sasa, ni kwamba mpaka kufikia mwaka 2030, wanalenga kuhakikisha nyama nyeupe



Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde (kulia), akimkabidhi kuku Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga Elberto Sanga, kwa ajili ya kuvipatia vikundi vya wafugaji. **PICHA: YASMINE PROTACE**

inapatikana kwa kiasi kikubwa.

"Bila ya kuwapo elimu yoyote ya usugaji ifikapo mwako 2030, nyama nyeupe haitakuwapo na takarukwapo na upungufu wanjamama (nchini)." anasema.

Anafafanua kuwa, mbali na kutoa elimu ya usugaji, pia wanasiambaza elimu itakayosaidia kuwahudumia kuku watakanakuwa wanaumwa.

Nandonde anasema, hadi sasa
wizara yake imeshaanza kuzali-
sha dawa za chanjo za kuwasaid-
ia wafugaji, hasa panapoibuka
magonjwa ya mdondo.

Mkurugenzi huyo anasema
mdondo una kawaida ya ku-

wakumba kuku kila mara, la-
kirikukosa elimu kwa wafugaji
wamekuwa wakitumia mbinu
potofu ya kuwapatia kuku ma-
jani, wakidhani kuwa ni dawa
mbadala.

* Kwa mujibu wa Nandonde, mradhi hadi sasa unaendelea kujikita kutoa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Dodoma, Singida na wilayani Mkuranga, mkoa wa Pwani.

Anadokeza kinachofanyika sasa ni mukakati wa kugawa bure kuu kwa vikundi vya wafugaji ikiwa ni namna ya kuinua hapa masa za ufugaji katika jamiili Mkuranga ukiwa mfano mo

jwapon.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvvi, Abdallah Ullega, anasema mwaka jana walikabidhi kuku kwa baadhi ya watu, lakin walipowatembelea, baadhi hawakukutwa nayo.

"Umekabidhiwa kuku, ni fedha ya serikali. Hivyo, unatakiwa kuwanunza," anasema Ulega, akidokeza ni mwelekeo unaowawajibisha wafugaji wab-adilike kiuchumi.

Tahadhari nyingine ya Naibu Waziri huyo ni kwamba kuku hao wasitumike kinyume, iki-wamo kuwachinja.

"Baada ya miezi mitatu tuta-

watembelea katika vikundi na watakoakutwa wanaendelea vizuri, watapewa kuku mara mbili yake," anasema.

Mary Makolele, ni mfugaji kuku wa Mkuranga, anayewahimiza wenzake kujungatikati shughuli za ufugaji, kuwaongezza kipato.

Anaipongeza serikalikwa kuwapatia mikopo hiyo ya misfugisisiyo na riba, huku akiwatake wenzake wajitahidi kuufuga kwnamna ya kujiongezea kipato nisiri ya masfanikio ni kila anaypatiwa misfugo, aismamie zuri, ili waionegezea manufaa kipato.

Nazee *

nabaraza hayo kulkutana majukumu yao.
aka wazee kuwashiriksha attika mabaraza hayo na oe mchango yao.
huyo allimponeza Rais i kwa kutla salini sheria in-
su wazee ambayo itairma-
awl wa wao kwa maslahi
a yao.
Mratibu wa Miradi wa Ju-
ni Wazee (JUWAZA), Hall-
i allimponeza wilaya hiyo
uzi wa kufanya uzinduzi
raza hayo ili kuweshezhi
ipate stabiki zao.
pande wao wazee, wal-
itashirkiana katika kue-
mabaraza hayo ili
apate haki yake katika



imataifa ya Golden

Ilevya

iji, wasambazaji na lawa za kulevyia, lili-
iumiwa huyo na kuse-
va mahakamani mara
zapokamilika.
itaka vijana kuacha
ta biashara ya dawa
va kuwa wanaangam-
zi ya talifa badala yake
ghuli halali wafanye.

Waanika dagaal waomba msaada

**Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Chama
cha Waanika Dagaal wa
eneo la Mangapwani, Mo-
hammed Omar Makame,
ameiomba serikali
kuwasaidia kuwatatalia
changamoto zinazowaka-
bili ikiwamo ya kuwajen-
gea sehemu ya kuhifa-
dhia mizigo yao.

Akizungumza na
waandishi wa habari
jana, alisema kutatuliwa
kwa changamoto hizo
kutawasaidia kupata
sehemu ya uhakika wa
kuanika pamoja na ku-
pata sehemu ya uhakika
ya kuhifadhi mizigo yao.

Pia alisema katika
eneo hilo wanakabiliwa
na tatizo la majisafi na
salama na uchache wa
vyoo nya kudumu, jambo
ambalo linahatarisha
usalama wa afya zao.

"Tatizo hili tumeshal-
ipeleka ofisi za hal-
mashauri ya wilaya hadi
mkoa, lakini bado limeku-
wa likiendelea. Tunaomba
kusaidiwa ili tufanye kazi
zetu kwa amani zaidi,"
alisema.

Mwenyekiti huyo
aliomba serikali kuangal-
iwa upya bei elekezi ya
dagaal kama iliyowekewa
katika zao la mwani na
Kuwashauri wapishi wa
dagaal kuweka mfumo wa
kutumia majiko ya gesi ili
kuhifadhi mazingira.

"Miti imekuwa ikihu-
jumiwa sana hivi kutumia
nishati ya gesi itasaidia
kupunguza uharibifu wa
mazingira ya ukataji wa
miti ovyo," alisema.

Naye Subira Faki Kom-
bo, mfanyabiashara wa
kuanika dagaal, alisema
kuwa po kwa ghala la
kuhifadhi mizigo kuta-
wanufaisha waanika da-
gaa kuondokana na tatizo
la wizi wa vitu vyao
wanavyofanyia kazi.

Aliomba serikali
kuliangalia suala hilo na
kwamba kazi hiyo inawa-
saidia kukidhi mahitaji ya
familia zao na wengine
wamekuwa na hali ngumu
na ni wajane.

Pamoja na hayo, ali-
omba serikali kuwapatia
mikopo isiyo na riba ili
kuwasaidia kujinyanyua
zaidi kimaisha kwa ku-
fanya blashtara itayoweza
kuwanyanyua zaidi na
kuijendeleza kimaisha
bila ya kuhitaji msaada.

TABORA UNGUJA

TABORA

Mkuu wa Mkoa awashukia DC, DED migogoro ya wakulima, wafugaji

Na ABDALLAH AMIRI

MKUU wa Mkoa (RC) wa Tabora, Philemon Sengati ametoa mwezi moja kwa Mkuu wa Wilaya (DC) ya Igunga, John Mwaipopo na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya (DED), Revocatus Kuuli kuhakikisha wanatatuwa migogoro ya wakulima na wafugaji wa Kitongoji cha Magogo, Kata ya Isakamaliwa na Kijiji cha Makomero, Kata ya Igunga mjini.

Alditoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa wilaya hiyo kwenvye mikutano wa hadharu uliofanyika katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine akiwa katika ziara yake ya siku moja ya kukagua shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoa na kujitambulisha kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Akizungumza na umati wa wananchi hao.

Sengati aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali yao kwa kufanya kazi kwa bidi kwa kuwa Rais Dk. John Magufuli amekuwa akihimiza wananchi kufanya kazi kwa bidi.

Alisema Wilaya ya Igunga inayo mabonde mengi ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliani ikiwemo skimu ya umwagiliani kilimo cha mpunga Mwanzugi, ambapo mabonde hayo yakitumia vizuri itasaidia wananchi kujipatia kipato cha kutosha.

Aidha alitoa wito kwa watumishi kuacha tabia ya kudharau wananchi ikiwa ni pamoa kutokula fedha za Serikali na zinazochangwa na wananchi kwa shughuli za maendeleo.

Hata hivyo aliwataka wananchi watoe kero zao walizonazo ambapo mkulima Ally William wa Kijiji cha Isakamaliwa, alimweleza kuwa

ye ye ni mkulima wa kilimo cha umwagiliani na analima hekari nane za mahindi.

Pamoja na hilo alisema hivi sasa wafugaji wamekuwa wakiwatishia kuwaua kwa kuwaamchia tawakala makoromeo.

"Mhesimiwa mkuu wa mkoa mwaka 2014 zaidi ya wakulima wenzetu saba waliuawa na wafugaji, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa na viongozi, hivyo hali hiyo imeanza tena kujirudia, tunaomba utusaidie," alisema William.

Naye Nyiga Nyanda wa Kijiji cha Makomero alimwambia mkuu wa mkoa kuwa mbuga ya Wembere imetengenishwa na wakulima na wafugaji, lakini baadhi ya wafugaji wamejenga katika maeneo ya wakulima jambo ambalo limekuwa na migogoro ya mara kwa mara.

Baada ya kusikiliza kero hizo kutoka kwa wananchi. Sengati alisema: "kwa kweli nimesononeka sana kusikia kuwa kuna wakulima miaka ya nyuma waliuawa na wafugaji, kweli imeniumiza sana."

"Ndugu zangu wananchi, nataka kuwaamchia ukiona kuna migogoro ujue eneo hilo viongozi wake hawawayibiki ipasavyo, hivyo leo natao maelekezo mkuu wa wilaya na mkurugenzi nataka ndani ya mwezi mmoja mniipe mpango kazi wenu kwa maandishi juu ya utatuzi wa migogoro hiyo ya wakulima na wafugaji," alisema Sengati.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Igunga, Mwaipopo alimhakikisha mkuu huyo wa mkoa kuwa watashughulikia suala hilo ndani ya mwezi mmoja na kultolea taarifa kwa maandishi.

- PICH: MPIGAPICHA WETI

/ to the expenses.

THE GUARDIAN

will be taking and 500 students will be for short courses," Masunga said.
Page 4

Extreme weather disrupts fishing activities in Tanga

By Guardian Correspondent, Tanga

EXTREME weather conditions, cooler temperatures and strong winds are among the factors currently affecting fishing activities in Tanga Region's Exclusive Economic Zone (EEZ) of the Indian Ocean.

The situation is also said to affect businesses at the Kasera and Chumbageni major fish markets due to shortage of fish. The cooler temperatures are not suitable for fish move more when the pressure is changing.

Investigations by this paper revealed that some fishermen are now avoiding conducting fishing activities in the Indian Ocean over fears of being hit by strong winds and high waves.

One of the fishermen, Ally Saleh who conducts businesses at the Kasera fish market said the situation started to change early this month due to extreme weathers which include cold conditions and strong winds.

"We are currently experiencing strong winds and prolonged cooler temperatures which are not suitable for us; most fishers cannot go into the sea when there are strong winds. We are conducting our activities in a difficult environment," said Saleh.

"Some few fishermen attempted to go into the sea; they were hit by high waves and lost control of the fishing canoe. They stayed in the Indian Ocean for more than two days," he said.

Ramadhani Bashiru said: "We are all worried; the ongoing extreme weather and high waves threaten our lives."

He said most of the residents depend on fish for food and business especially the Uwono Msumari and Bangara species which become plenty available during hotter seasons. He said most of the fish species become rare during cooler temperatures.

Some of the women selling fried fish and sardines at the markets said the current weather has resulted in poor supply of fish, the situation which has contributed to fish prices going up.

Sara Mdingo said: "The prices are too high that some of us cannot afford. A small bucket of sardines is sold at a price of between 45,000/- and 48,000/-."

According to Sara they were previously buying a bucket of sardines at a price of between 18,000/- and 25,000/-.

"I have stopped selling fried sardines until there is a stable supply," said Sara.

Recently, the Tanzania Meteorological Authority (TMA) warned of strong winds and high waves in the Indian Ocean coastal areas and the country's great lakes, saying the situation is likely to disrupt fishing activities and marine transport.

TMA said strong winds reaching 50 kilometers per hour and high waves reaching 3.8 meters were expected over the entire coastal area of Lindi, Mtwara, Tanga and Dar es Salaam.

The TMA weather forecast added that the rough weather was also expected to hit Tanzania's Zanzibar twin Islands of Pemba and Unguja.

According to the forecast, strong winds reaching 50 kilometers per hour were expected in Lakes Victoria, Nyasa and Tanganyika.

“

This is an opportunity for our industries to develop, let me call upon Tanzanians to invest in essential products so that they could be supported by the government

Pregnancy trend prompts leaders to act

DAILY NEWS Page 5.



TABORA Regional Commissioner, Dr Philemon Sengati (fourth right), is briefed on fish production from an officer in charge of Mwamapuli Fish Ponds Centre, Mr Joachim Barhe, during his tour of Igunga District in Tabora Region yesterday. (Photo by Daudi Tiganya)